# UFUNUO 4



COMIC BIBLE SOCIETY

Published by the Comic Bible Society, LLC
Copyright © 2023

Kingstone Comics maintains copyright to this comic book as provided by United States copyright law.

Print and digital copies of this version may be freely distributed without penalty under a Creative Commons license.


NJOO, NITAKUONYESHA HUKUMU YA YULE KAHABA MKUU [1] AKETIYE JUU YA MAJI MENGI.
WAFALME WA NCHI WAMEZINI NAYE, NAO WAKAAO KATIKA NCHI WAMELEVYWA KWA MVINYO YA UASHERATI WAKE. [2]
"MALAIKA AKANICHUKUA KATIKA ROHO HATA JANGWANI."
" PALE NIKAONA MWANAMKE, AMEKETI JUU YA MNYAMA MWEKUNDU SANA, MWENYE KUJAA MAJINA YA MAKUFURU, MWENYE VICHWA SABA NA PEMBE KUMI."
"MWANAMKE YULE ALIKUWA AMEVIKWA NGUO YA RANGI YA ZAMBARAU, NA NYEKUNDU, AMEPAMBWA KWA DHAHABU, NA KITO CHA THAMANI, NA LULU."
"ALISHIKA KIKOMBE CHA DHAHABU MKONONI MWAKE, KILICHOJAWA NA MACHUKIZO, NA MACHAFU YA UASHERATI WAKE." [3]
"ALIKUWA NA JINA LIMEANDIKWA KWENYE KIPAJI CHA USO WAKE..."
LA SIRI BABELI MKUU MAMA WA MAKAHABA NA MACHUKIZO YA DUNIANI.
[1] ILIKUWA DESTURI KWA MAKAHABA WA KIRUMI KUVAA KILEMBA CHA KICHWA NA MAJINA YAO.
[2] MAKAHABA KWA MARA NYINGI WALIVALIA NGUO ZA THAMANI NA VITO KUWAVUTIA WAATHIRIWA WAO, KWA HIYO DINI HII YA UONGO INAJIVIKA KUYAVUTIA MATAIFA YOTE YAWE CHINI YA NGUVU ZAKE.
[3] NI MAMA YA MAKAHABA KWA SABABU DINI ZOTE HATIMAYE ZATOKA BABELI.
[4] DINI ZA UONGO ZIMEUA UMATI NA MFUMO HUUWA DINI YA UONGO YA MWISHO ITAKUWA MBAYA ZAIDI KULIKO ZOTE.
"ALIKUWA AMELEWA KWA DAMU YA WATAKATIFU..." [4]
UFUNUO 17:1-6




[1] YULE MNYAMA (MPINGA KRISTO) ATANGA MKONO KABISA MFUMO HUU WA KIDINI WA UONGO (YULE KAHABA.) MFALME NA MFALME

[2] ISTILAHI "ALIYEKUWA, ASIYEKUWAPO, NA ATAKAYEKUJA," INAASHIRIA KUWA BAADA YA "KUFUFUKA" KWAKE MPINGA KRISTO ATAPAGAWA NA PEPO MKUU KUTOKA

UFUNUO 17:6-8






UFUNUO 17:9-11


VICHWA SABA NI WAFALME KUMI [1] AMBAO BADO HAWAJAPOKEA UFALME LAKINI WATATAWALA KWA LISAA LIMOJA [2] PAMOJA NA YULE MNYAMA.
WATAFANYA VITA DHIDI YA MWANA-KONDOO - LAKINI MWANA-KONDOO ATAWASHINDA KWA KUWA YEYE NI BWANA WA MABWANA NA MFALME WA WAFALME.
SASA KWA KUWA TUMEUNGANISHA UWEZO, HATUHITAJI TENA MFUMO HUU WA KIDINI.
MWANGAMIZE.
"YULE MNYAMA NA ZILE PEMBE KUMI WATAMCHUKIA YULE KAHABA NA KUMUANGAMIZA..." [3]
[1] UFALME WA MPINGA KRISTO UTAGAWANYWA KATIKA WILAYA KUMI ZA UTAWALA ZINAZOMILIKIWA NA VIONGOZI KUMI.
[2] BIBILIA YASEMA WAKATI WAO UTAKUWA MFUPI. LISAA LIMOJA LINAASHIRIA WAKATI MFUPI WA MIAKA MITATU NA NUSU WATAKAOTAWALA NA MPINGA KRISTO.
[3] LAKINI WATAKAPOKUJA KUMILIKI WATAANGAMIZA MFUMO WA UONGO WA KIDINI ULIOWASAIDIA KUPATA MAMLAKA.
UFUNUO 17:12-18




[1] BAADA YA MALAIKA WA TANO KUUTUMBUKIZA ULIMWENGU KATIKA GIZA, FAHARI YA MALAIKA HUYU ITASHIKA UMAKINI WA WATU WA ULIMWENGU.

[2] BABELI YA KIDINI YAVUTIA MATAIFA KUINGIA KWENYE ULEVI WA KIROHO NA MIUNGU YA UONGO.

[3] BABELI YA KIBIASHARA INATONGOZA WATU NA MATAIFA NA MUNGU WA UONGO WA KUPENDA MALI.

[4] LAKINI MUNGU MWENYEWE AHUKUMU MFUMO WA UONGO WA BABELI.

[5] KAMA BABELI YA ZAMANI ILIVYOANGUKA KWA SIKU MOJA CHINI YA HUKUMU YA MUNGU, NDIVYO BABELI YA KISASA ITAKAVYOANGUKA SIKU MOJA.




KISHA KULIKUWA NA SAUTI NYENGINE MBINGUNI ILIYOSEMA---
TOKENI KWAKE ENYI WATU WANGU MSISHIRIKI MAPIGO YAKE.
DHAMBI ZAKE ZIMEFIKA HATA MBINGUNI NA MUNGU AMEKUMBUKA MAOVU YAKE.
MLIPENI MARA MBILI KWA KADIRI YA MATENDO YAKE. KATIKA KIKOMBE CHAKE MCHANGANYISHIENI MARADUFU. [4]
KWA SABABU HIYO MAPIGO YAKE YATAMKUMBA KATIKA SIKU MOJA: MAUTI, NA HUZUNI, NA NJAA. [5]
ATAANGAMIZWA NA MOTO KWA KUWA BWANA ANAYEMUHUKUMU NI MKUU.


UFUNUO 18:1-8


"WAFALME WA DUNIA NA WAFANYA BIASHARA WATAKAPOYAONA HAYA YOTE WATALIA NA KUHUZUNIKA NA KUTOA SAUTI."
OLE! OLE MJI ULE MKUU, WENYE NGUVU WA BABELI, KWANI ADHABU YAKO IMEKUJA KWA LISAA LIMOJA!
OLE, OLE, MJI ULE ULIO MKUU, AMBAMO NDANI YAKE WOTE WENYE MERIKEBU BAHARINI WALIPATA MALI KWA UTAJIRI WAKE! KWANI KATIKA SAA MOJA AMEFANYWA UKIWA.
[1] KWA KUANGUKA KWA BABELI, MAISHA NA HALI YOYOTE YA KAWAIDA YATAKATIZWA KABISA. HAKUTAKUWA NA MUZIKI, VIWANDA, UANDALIZI WA CHAKULA (JIWE LA KUSAGIA), STIMA AU HATA HARUSI.
[2] MFUMO WA KIOVU WA DINI YA UONGO PAMOJA NA BABELI YA KIBIASHARA NA KISIASA ZITAKUWA ZIMETENDA UKATILI WA KUTISHA DHIDI YA WATU WA MUNGU. MUNGU MWENYEZI ATAHUKUMU KABISA MFUMO WA KIDINI, KIBIASHARA NA KISIASA KATIKA MAANDALIZI YA KURUDI KWA MFALME WA HAKI - YESU KRISTO.


UTAJIRI NA UFAHARI WAKO WOTE UMEPOTEA - HAUTAWAHI KUPATIKANA TENA.
KATIKA LISAA LIMOJA TU UTAJIRI WA AJABU UMEANGAMIZWA!
KAMA HIVI KWA VURUGU NYINGI MJI MKUU WA BABELI UTATUPWA CHINI.
MUZIKI...MAWE YA KUSAGIA...SAUTI YA MABWANA HARUSI NA BI HARUSI HAITASIKIWA NDANI YAKO TENA KABISA. [1]
HAKUNA FUNDI ATAPATIKANA NDANI YAKO NA NURU YA TAA HAITAWAHI KUNG'AA NDANI YAKO TENA.
KWA UCHAWI WAKO MATAIFA YOTE YALIPELEKWA MRAMA.
NDANI YAKE ILIONEKANA DAMU YA MANABII NA WATAKATIFU NA WOTE WALE WALIOUAWA JUU YA NCHI. [2]
UFUNUO 18:9-24




[1] KITANI SAFI INASIMAMIA MATENDO MATAKATIFU YA WATAKATIFU.

[2] BIBILIA INAKATAZA KUABUDU MALAIKA. MUNGU PEKEE NDIYE ANAYESTAHILI KUABUDIWA.




UFUNUO 19:1-10




[1] MAJENERALI WA KIRUMI WALIPORUDI NA USHINDI WANGEPANDA FARASI MWEUPE WA VITA KATIKA MAANDAMANO YA USHINDI. YESU KRISTO ALIKUJA WAKATI WA KWANZA KWA UNYENYEKEVU JUU YA MWANA PUNDA LAKINI WAKATI WA PILI ARUDI KWA USHINDI JUU YA FARASI MWEUPE.

[2] HAKUNA KINACHOMPITA KRISTO, KUZIFANYA HUKUMU ZAKE ZOTE SAHIHI NA ZA HAKI.

[3] VAZI LILOLOWA DAMU LINAASHIRIA VITA VIKUU ALIVYOPIGANA NA KUSHINDA DHIDI YA DHAMBI, IBILISI, NA KIFO. HII SI KUTOKA KWA VITA VYA HAR-MAGEDONI KWANI HAIJATOKEA BADO.

[4] JESHI LILILOKO NAYE HALIRUDI NA KRISTO KUFANYA VITA KWANI HAWANA SILAHA, ILA KUMILIKI NAYE BAADA YA YEYE KUWASHINDA ADUI WAKE WOTE.


KING of KINGS
LORD of LORDS



NJOONI MKUTANE KWA KARAMU YA MUNGU ILIYO KUU, ILI MPATE KULA NYAMA YA WAFALME, NA NYAMA YA MAJEMADARI, NA NYAMA YA WATU HODARI, NA NYAMA YA FARASI NA YA WATU WAWAPANDAO, NA NYAMA YA WATU WOTE, WAUNGWANA KWA WATUMWA, WADOGO KWA WAKUBWA. [1]
KISHA NIKAMWONA HUYO MNYAMA, NA WAFALME WA NCHI, NA MAJESHI YAO, WAMEKUTANA KUFANYA VITA NA YEYE AKETIYE JUU YA FARASI YULE NA MAJESHI YAKE.
[1] MUNGU ATANGAZA USHINDI HATA KABLA VITA HAVIJAANZA.



"LAKINI YULE MNYAMA AKAKAMATWA, NA YULE NABII WA UONGO PAMOJA NAYE, YEYE ALIYEZIFANYA HIZO ISHARA KWA NIABA YAKE. KWA HIZO ALIWADANGANYA WATU WALE WALIOIPOKEA ILE CHAPA YA HUYO MNYAMA, NAO WALIOISUJUDIA SANAMU YAKE NA ISHARA HIZO."
"WOTE WAWILI WAKATUPWA WANGALI HAI KATIKA LILE ZIWA LA MOTO LIWAKALO KWA KIBERITI."
"NA WALE WALIOSALIA WALIUAWA KWA UPANGA WAKE YEYE ALIYEKETI JUU YA YULE FARASI, UPANGA UTOKAO KATIKA KINYWA CHAKE, NA NDEGE WOTE WAKASHIBA KWA NYAMA ZAO."[1]
[1] MAJESHI YA MPINGA KRISTO NA WENYE DHAMBI WALIOSALIA DUNIANI WAUAWA, KUASHIRIA MWISHO WA WAKATI WA DHIKI.
UFUNUO 19:20-21



"KISHA NIKAONA MALAIKA AKISHUKA KUTOKA MBINGUNI MWENYE UFUNGUO WA KUZIMU NA NYORORO KUBWA MKONONI MWAKE."
[1] WAKATI WA UMILIKI WA KRISTO WA MIAKA ELFU MOJA DUNIANI IBILISI AFUNGWA GEREZANI.



AKAMSHIKA YULE JOKA--YULE NYOKA WA ZAMANI, AMBAYE NI IBILISI NA SHETANI--NA AKAMFUNGA MIAKA ELFU..." [1]
"...NA AKAMTUPA KATIKA KUZIMU, AKAMFUNGA, AKATIA MUHURI JUU YAKE, ASIPATE KUWADANGANYA MATAIFA TENA, HATA ILE MIAKA ELFU ITIMIE." [1]
"BAADA YA HAYO YAPASA AFUNGULIWE KWA MUDA MCHACHE."



"NIKAONA VITI VYA ENZI, WALIPOKETI JUU YAKE WALE WALIOPEWA MAMLAKA YA KUHUKUMU."
"NAMI NIKAONA ROHO ZAO WALIOKATWA VICHWA KWA AJILI YA USHUHUDA WA YESU NA KWA AJILI YA NENO LA MUNGU."
"HAWAKUMSUJUDIA YULE MNYAMA WALA SANAMU YAKE WALA HAWAKUIPOKEA ILE CHAPA KATIKA VIPAJI VYA NYUSO ZAO WALA KATIKA MIKONO YAO."
"WAKAWA HAI NA WAKATAWALA PAMOJA NA KRISTO MIAKA ELFU."
[1] WALIOKOMBOLEWA KATIKA ZAMA ZA KANISA, WATAKATIFU WA AGANO LA KALE, MASHAHIDI WA DHIKI NA WAUMINI WA DHIKI WATAKAOSALIA SASA WANA MILI ILIYOFUFUKA KUMILIKI NA KRISTO.
[2] UFUFUO WA KWANZA NI UFUFUO WA WAUMINI. MILI YA WAUMINI HAITAFUFULIWA (UFUFUO WA PILI) MPAKA HUKUMU YA KITI CHEUPE KIKUU CHA ENZI.


"HAO WAFU WALIOSALIA HAWAKUWA HAI HATA ITIMIE ILE MIAKA ELFU. HUO NDIO UFUFUO WA KWANZA." [1]
"HERI, NA MTAKATIFU, NI YEYE ALIYE NA SEHEMU KATIKA UFUFUO WA KWANZA. [2] JUU YA HAO MAUTI YA PILI HAINA NGUVU, BALI WATAKUWA MAKUHANI WA MUNGU NA WA KRISTO NAO WATATAWALA PAMOJA NAYE HIYO MIAKA ELFU."
UFUNUO 20:4-6


"NA HIYO MIAKA ELFU ITAKAPOKWISHA, SHETANI ATAACHILIWA KUTOKA GEREZANI MWAKE."
"NA NIKAWAONA WAKIPANDA JUU YA UPANA WA NCHI, WAKAIZINGIRA KAMBI YA WATAKATIFU, NA MJI HUO ULIOPENDWA." [2]
[1] GOGU NA MAGOGU NI MAJINA YALIYOPEWA WAASI NA MKUBWA WAO WANAPOANDAMANA KWA UKAIDI DHIDI YA KRISTO NA UONGOZO WAKE. MAGOGU ALIKUWA MJUKUU WA NUHU (MWANZO 10:2) ALIYEKUWA MWANZILISHI WA UFALME WA ZAMANI. INAWEZEKANA GOGU NI JINA LA KIONGOZI HUYU WA UASI ANAYEONGOZA JESHI LAKE LIJULIKANALO KAMA MAGOGU.
[2] YERUSALEMU ITAKUWA MJI MKUU AMBAPO KRISTO ATATAWALA WAKATI WA MIAKA ELFU.
[3] KUSONONEKA KUSIKO NA MWISHO WALA NAFUU KUTAKUWA HALI YA MWISHO YA IBILISI, MALAIKA WALIOASI - PAMOJA NA WAKE NA WAUME WOTE AMBAO HAWAKUOKOLEWA.


"NAYE ATATOKA KUWADANGANYA MATAIFA WALIO KATIKA PEMBE NNE ZA NCHI, GOGU NA MAGOGU, KUWAKUSANYA KWA VITA. [1] AMBAO HESABU YAO NI KAMA MCHANGA WA BAHARI."
"LAKINI MOTO UKASHUKA KUTOKA MBINGUNI UKIYASHAMBULIA MAJESHI NA UKAWALA."
"NA YULE IBILISI, MWENYE KUWADANGANYA, AKATUPWA KATIKA ZIWA LA MOTO NA KIBERITI, ALIMO YULE MNYAMA NA YULE NABII WA UONGO, NAO WATATESWA MCHANA NA USIKU HATA MILELE NA MILELE." [3]
UFUNUO 20:7-10


KISHA NIKAONA KITI CHA ENZI KIKUBWA NA YEYE AKETIYE JUU YAKE. [1] NCHI NA MBINGU ZIKAKIMBIA USO WAKE, NA MAHALI PAO HAPAKUONEKANA. [2] NIKAWAONA PIA WAFU, WAKUBWA KWA WADOGO, WAMESIMAMA MBELE YA HICHO KITI CHA ENZI; NA VITABU VIKAFUNGULIWA."
"NA KITABU KINGINE KIKAFUNGULIWA, AMBACHO NI CHA UZIMA [3], NA HAO WAFU WAKAHUKUMIWA KATIKA MAMBO HAYO YALIYOANDIKWA KATIKA VILE VITABU, SAWASAWA NA MATENDO YAO."
"BAHARI IKAWATOA WAFU WALIOKUWAMO NDANI YAKE, NA MAUTI NA KUZIMU ZIKAWATOA WAFU WALIOKUWAMO NDANI YAKE, NA WAKAHUKUMIWA, KILA MTU KWA KADIRI YA MATENDO YAKE." [4]
[1] HUKUMU YA KITI KIKUU CHEUPE CHA ENZI NI HUKU YA MWISHO YA WASIOAMINI WOTE WA ZAMA ZOTE.
[2] MTUME YOHANA ANASHUHUDIA ULIMWENGU ULIOHARIBIWA NA DHAMBI UKIANGAMIA. HII PIA INATABIRIWA NA MTUME PETERO (II PETERO 3:10-13).
[3] KITABU CHA UZIMA KINA REKODI YA WALE WOTE WALIOKOMBOLEWA.
[4] WOTE WATAHUKUMIWA KULINGANA NA MAWAZO YAO (LUKA 8:17), MANENO (MATH.12:37) NA MATENDO (MATH. 16:27).
[5] HAKUNA NAFASI YA PILI. UAMUZI WOWOTE MTU ALIONAO KABLA YA KIFO CHAKE UTAMFUATA HADI KITI CHA ENZI CHA MUNGU KWA HUKUMU. MOJAWAPO YA UKWELI WA KUTISHA NA WA UCHUNGU KATIKA BIBILIA NI KUWA MTU ANAPOKUFA NJE YA KRISTO, JEHANAMU NI MAKAAZI YAKE MILELE. WENYE DHAMBI WOTE WA UMRI WOTE, BINAADAMU NA MAPEPO, WAKO KATIKA ZIWA LA MOTO MILELE. INATISHA SANA KWA WAKRISTO NA WASIO WAKRISTO KUELEWA, LAKINI TUNAJUA KWA UKWELI WA NENO LA MUNGU KUWA HUU NDIO MWISHO UNAOWANGOJEA UMATI WA WATU. YESU ALISEMA, " NJIA NI PANA IENDAYO UPOTEVUNI, NAO NI WENGI WAIINGIAO."




"MAUTI NA KUZIMU ZIKATUPWA KATIKA LILE ZIWA LA MOTO. HII NDIYO MAUTI YA PILI, NA IWAPO MTU YEYOTE HAKUONEKANA AMEANDIKWA KATIKA KITABU CHA UZIMA, ALITUPWA KATIKA LILE ZIWA LA MOTO." [5]


"KISHA NIKAONA MBINGU MPYA NA NCHI MPYA, KWA MAANA MBINGU ZA KWANZA NA NCHI YA KWANZA ZIMEKWISHA KUPITA, WALA HAPANA BAHARI TENA."
"NAMI NIKAUONA MJI ULE MTAKATIFU - YERUSALEMU MPYA.[1] ULISHUKA KUTOKA MBINGUNI KWA MUNGU. ULIWEKWA TAYARI, KAMA BIBI-ARUSI ALIYEKWISHA KUPAMBWA NA KUVIKWA ILI KUKUTANA NA MUMEWE."
"NIKASIKIA SAUTI KUBWA KUTOKA KATIKA KILE KITI CHA ENZI: 'TAZAMA, MASKANI YA MUNGU NI PAMOJA NA WANADAMU! ATAFANYA MASKANI YAKE PAMOJA NAO, NAO WATAKUWA WATU WAKE, NAYE MUNGU MWENYEWE ATAKUWA PAMOJA NAO.'"
"NAYE ATAFUTA KILA CHOZI KATIKA MACHO YAO. WALA MAUTI HAITAKUWAPO TENA - WALA MAOMBOLEZO, WALA KILIO, WALA MAUMIVU HAYATAKUWAPO TENA. MAMBO YA KWANZA YAMEKWISHA KUPITA."
"NA YEYE AKETIYE JUU YA KILE KITI CHA ENZI AKASEMA, 'TAZAMA, NAYAFANYA YOTE KUWA MAPYA!' PIA AKANIAMBIA, 'ANDIKA YA KWAMBA MANENO HAYO NI YA KWELI NA YA KUAMINIKA.'"
[1] MJI MKUU WA MBINGUNI.
[2] BIBILIA, KANDO NA KUTAJA KUTOAMINI, PIA INATOA TABIA NA SIFA ZA MITINDO YA MAISHA YA WASIOAMINI.
[3] NA KUNA MWISHO MMOJA PEKE YAKE KWA WASIOAMINI - JEHANAM. NA NI MILELE NA MILELE BILA NAFASI NYENGINE AU KIPENYO CHA KUTOROKA.


" PIA AKASEMA,' IMEKWISHA KUWA! MIMI NI ALFA NA OMEGA, MWANZO NA MWISHO. MIMI NITAMPA YEYOTE MWENYE KIU RUHUSA YA KUNYWA KUTOKA KWA CHEMCHEMI YA MAJI YA UZIMA, BURE. '"
"BALI WAOGA, WASALITI, NA WASIOAMINI, NA WACHUKIZAO, NA WAUAJI, NA WAZINZI, NA WACHAWI, NA HAO WAABUDUO SANAMU, NA WAONGO WOTE, [2]
"MWISHO WAO NI KATIKA LILE ZIWA LIWAKALO MOTO NA KIBERITI - HII NDIYO MAUTI YA PILI." [3]
UFUNUO 21:1-8


MMOJA WA WALE MALAIKA SABA WALIOKUWA NA VILE VITASA SABA AKANICHUKUA KATIKA ROHO MPAKA MLIMA MKUBWA MREFU. NA KWA MSHANGAO HAPO NIKAUONA ULE MJI MTAKATIFU, YERUSALEMU, UKISHUKA KUTOKA MBINGUNI KWA MWENYEZI MUNGU.
MWANGAZA WAKE MJI ULE ULIKUWA MFANO WA KITO CHENYE THAMANI NYINGI. ULINGAA HASWA KWA UTUKUFU WA MUNGU.
[1] KAMA TU LULU ZA KIDUNIA ZINAVYOTENGEZWA KWA KUJERUHIWA KWA NGOZI YA CHAZA - VILE VILE MILANGO HII MUKII YA LULU ITAWAKUMBUSHA WAUMINI MILE NA MILELE JUU YA UKUU WA KUTESEKA KWA KRISTO KWA NIABA YAO.




UFUNUO 21:9-27


"HAKUNA HEKALU NDANI YAKE KWA MAANA BWANA MUNGU MWENYEZI NA MWANA-KONDOO NDIO HEKALU NDANI YA MJI."
"WALA HAUHITAJI JUA WALA MWEZI KUUANGAZA, KWA MAANA UTUKUFU WA MUNGU HUUTIA NURU, NA TAA YAKE NI MWANA-KONDOO."
"NA MATAIFA YA ULIMWENGU WATATEMBEA KATIKA NURU YAKE NA WAFALME WA NCHI KULETA UTUKUFU NA FAHARI YA MATAIFA YAO NDANI YAKE."


"MILANGO YAKE HAITAFUNGWA KAMWE NA HUMO HAMNA USIKU."
NDANI YAKE HAKITAINGIA KAMWE CHO CHOTE KILICHO KICHAFU WALA WAONGO WOWOTE WALA WALE WAFANYAO MATENDO YA MACHUKIZO.
" WALIO WALIOANDIKWA MAJINA YAO KATIKA KITABU CHA UZIMA CHA MWANA-KONDOO TU NDIO WALIOKUBALIWA KUINGIA MJINI."
UFUNUO 21:22-27


KISHA MALAIKA ALIPOKUWA AKINIONYESHA VITU HIVI, NILIONA MTO WA MAJI YA UZIMA WENYE KUNG'AA KAMA BILAURI, UKITOKA KATIKA KITI CHA ENZI CHA MUNGU NA CHA MWANA-KONDOO. [1]
ULIPITA KATIKATI YA NJIA YA KATI YA MJI NA KWA PANDE ZOTE ZA ULE MTO, NILIONA MTI WA UZIMA.
MTI HUU UNAZAA MATUNDA AINA KUMI NA MBILI WENYE KUTOA MATUNDA YAKE KILA MWEZI - NA MAJANI YA MTI HUO NI YA KUWAPONYA MATAIFA.
LAANA YA DHAMBI HAITAKUWEPO MJINI.
WATUMISHI WAKE WATAMSUJUDU MUNGU NA MWANA-KONDOO KATIKA KITI CHAKE CHA ENZI.
JINA LAKE LITAKUWA KATIKA VIPAJI VYA NYUSO ZAO NAO WATAMWONA USO WAKE MUNGU. [2]
HAPATAKUWA NA USIKU TENA, WALA HAWANA HAJA YA TAA WALA YA NURU YA JUA - MUNGU ATAKUWA NURU YAO.
NAO WATATAWALA KAMA WAFALME - HATA MILELE NA MILELE.


[1] KWA KUWA HAKUNA MZUNGUKO WA KIHAIDROLOJIA KWA HII DUNIA MPYA, HAYA NI MAJI YA UZIMA YANAYOENDELEA KUTIRIRIKA KUTOKA KWA KITI CHA ENZI CHA MUNGU.
[2] KATIKA ULIMWENGU WA AWALI, HAKUNA BINADAMU ALIYEWEZA KUUONA USO WA MUNGU NA AISHI (KUTOKA 33:20-23). LAKINI SASA NA MILI MITUKUFU WAUMINI WAWEZA KUMTAZAMA MUNGU BILA MADHARA KWANI WAMEFANYWA WATUKUFU.
UFUNUO 22:1-5






UFUNUO 22:6-11


TAZAMA - NARUDI HIVI KARIBUNI!
NALETA TUZO LANGU NAMI NA NITAMPA KILA MTU KULINGANA NA ALICHOKIFANYA.
NI MWANZO NA MWISHO - WA KWANZA NA WA MWISHO.
HERI WAO WANAOFUA KANZU ZAO. WATAKUWA NA HAKI YA MTI WA UHAI NA WAWEZA KUINGIA NDANI YA MILANGO HADI NDANI MWA JIJI.
NJE YA MJI KUNA MBWA, WACHAWI, WAZINIFU, WAUAJI, WANAOABUDU MIUNGU NA WOTE WANAOPENDA NA KUTENDA UONGO.
MIE, YESU, NIMEMTUMA MALAIKA WANGU KUTOA USHUHUDA WA MAMBO HAYA KWA MAKANISA. MIMI NDIMI MZIZI NA KIZAZI CHA DAUDI. MIMI NDIYE NYOTA YA ASUBUHI INGAAYO.
"ROHO NA BI HARUSI WASEMA, 'NJOO!' MUACHE ANAYESIKIA ASEME, 'NJOO!'"
"NA KWA KILA ALIYE NA KIU MUACHE AJE KWANGU."
"NA KWA KILA ANAYETAMANI, MUACHE ACHUKUE BURE MAJI YA UZIMA."
UFUNUO 22:12-16




UFUNUO 22:18-21

"THE BIBLE EXPLAINED
IN EVERY LANGUAGE."








**SUPERBIBLE.TV**